## TAASISI YA VIWANGO YA ZANZIBAR (ZBS)

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Viwango ya Zanzibar Na.1 ya 2011.

Lengo kuu la kuanzishwa Taasisi ya Viwango ya Zanzibar ni kuhakikisha kuwa Zanzibar inakua na viwango vya bidhaa na huduma na kusimamia ubora wa bidhaa na huduma hizo. Viwango na bidhaa zenye ubora zinalenga kulinda afya na usalama wa watumiaji pamoja na kukuza uchumi wa Zanzibar na kuhifadhi mazingira ya nchi.

Taasisi ya Viwango ya Zanzibar (ZBS) inakaribisha maombi ya kujaza nafasi mpya kwa waombaji wenye sifa stahili katika Ofisi yake iliyopo Unguja kwa mwaka wa fedha 2026/2027; jumla ya nafasi hizo ni 03.

Nafasi yenyewe ni kama ifuatavo:-

1. **AFISA UKAGUZI NA UDHIBITI UBORA CHAKULA (FOOD) - DARAJA LA II (ZPSI-06) Nafasi 03**

**Sifa za muombaji:**

i. Awe ni Mzanzibari mwenye umri usiozidi miaka arobaini na tano (45).
ii. Awe mwenye Shahada ya Kwanza katika fani ya Sayansi ya Chakula (Food Science), Sayansi ya Mazingira (Environmental Science), Bailojia (Biology), Kilimo Mjumuisho (Agriculture General), Bioteknolojia (Biotechnology), Sayansi ya Udongo (Soil Science) au fani zinazolingana kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
iii. Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta.
iv. Uzoefu wa kazi ni sifa ya ziada.

**Majukumu**

i. Kufanya ukaguzi na kuchukua sampuli za bidhaa za chakula kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara.

ii. Kukusanya taarifa zitazotumika katika uandaaji wa mpango wa ukaguzi unaoendana na mfumo na kanuni za ukaguzi.
iii. Kuchukua sampuli za bidhaa za chakula za Mteja alieruhusiwa kutumia nembo ya ubora na cheti cha ubora kwa ajili ya ukaguzi.
iv. Kukusanya sampuli za lebo (batch) kwenye maeneo ya uingizaji wa bidhaa.
v. Kushiriki katika ukaguzi ili kuhakikisha ubora wa bidhaa zilizopatiwa cheti unakua endelevu.
vi. Kuweka kumbukumbu za ukaguzi wa bidhaa za chakula.
vii. Kutunza usalama wa vifaa anavyotumia wakati wa uchukuaji wa sampuli.
viii. Kukusanya taarifa zitakazotumika katika uandaaji wa ripoti ya utekelezaji ya robo, nusu na mwaka na kuwasilisha kunako husika.
ix. Kufanya kazi nyengine zinazolingana na majukumu yake kama atakavyopangiwa na Mkuu wake.

**NAMNA YA KUWASILISHA MAOMBI**

Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya kielektroniki kwenye mfumo wa maombi ya Ajira (ZanAjira) kupitia anuani ifuatayo:- http://portal.zanajira.go.tz si zaidi ya tarehe 14 Septemba, 2026 saa tisa na nusu alaasiri. Maombi hayo yaambatanishwe na vitu vifuatavyo:-

i. Maelezo binafsi ya muombaji (CV).
ii. Vivuli vya vyeti vya kumalizia masomo, kwa wale waliosoma nje ya nchi wanatakiwa kuwasilisha vyeti vyao vya uthibitisho kutoka TCU.
iii. Kivuli cha Cheti cha Kuzaliwa.
iv. Majina na anuani za Wadhamini wawili wanaotambulika.

**MAMBO YA KUZINGATIWA**

i. Muombaji atakaewasilisha "Statement of Result" au "Progressive Report" maombi yake hayatazingatiwa.
ii. Muombaji asiwe Muajiriwa wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
iii. Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-
**MKURUGENZI MKUU,**
**TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR,**
**S.L.P 1136,**
**ZANZIBAR.**
iv. Kwa msaada wa kitaalamu wasiliana na Taasisi ya Viwango Zanzibar kupitia email ajira@zbs.go.tz
Tangazo hili linapatikana pia katika Tovuti ya Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) ambayo ni **www.zbs.go.tz.**